

Kairuki aonyesha viwanda vyakula na mafuta ya kula kwa kujenga viwanda

Na Mwandishi Wetu,
MWANZA

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Uwekezaji), Angela Kairuki, amewataka wawekezaji na wafanyabiashara mkoani wa Mwanza kuchangamkia fursa ya uhaba wa vyakula vyamfugo na mafuta ya kula kwa kujenga viwanda ya kuchakata bidhaa hizo.

Kairuki amesema kwa kufanya hivyo wataondokana na uagizaji wa bidhaa hizo nje ya nchi.

Akihitimisha Mkutano wa Majadiliano kati ya serikali, wawekezaji na wafanyabiashara mkoani Mwanza kujadili changamoto na mapendekezo yanayolenga kuboresha mazingira ya biashara na kuvutia uwekezaji.

Waziri Kairuki alisema uwekezaji zaidi unahitajika katika eneo la chakula cha kuku na mafuta ya kula.

"Kuna uhitaji mkubwa wa viwanda vyakula kuzalisha chakula cha mifugo hasa kwa ukanda wa ziwa ambako kwenye idadi kubwa ya mifugo na uhitaji wake ni mkubwa, hivyo hii ni fursa kwenu kujengamkia," alisema Waziri Kairuki.

Alisema wizara yake kuititia Kituo cha Uwekezaji (TIC) wamejipanga katika kuzainishaa na kuzitambua fursa zote zilizopo ili zitangazwe kuwavutia wawekezaji wenye mitaji kuja kuwekeza ikiwamo kwenye viwanda vyakula cha mifugo.

"Tupo katika kutekeleza azma ya serikali ya kujenga uchumi wa kati na viwanda ifikapo 2025,

kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji ni sehemu ya kufanikisha azma hiyo," alisema Kairuki.

Alieleza kuwa serikali itaendelea kuwalinda wawekezaji, na wafanyabiashara wa ndani kwa kuhakikisha soko la ndani la bidhaa zinazozalishwa hapa nchini linahimarika na kuchochea ukuaji wa uchumi= kwa kasi inayostahili.

"Lengo letu ni kuachana na uagizaji wa bidhaa kutoka nje ya nchi jambo ambalo litaongeza ari ya uwekezaji katika viwanda vyakula bidhaa mbalimbali hapa nchini na kupunguza usafirishaji wa malighafi nje," alisema na kuongeza kuwa ajira zitaongezeka pia.

Aidha, Waziri Kairuki alisema Mkoani wa Mwanza ni moja ya mkoani ya kimkakati, hivyo wizara yake itatoa ushirikiano kwa

wawekezaji na wafanyabiashara kwa kuondolea kero zinakwamisha tukaji na maendeleo ya uwekezaji kwa kuwekeza mazingira rafiki na wezeshi kwa biashara.

Mwenyekiti wa TCCIA Mkoa wa Mwanza, Leopard Lema, alipongeza majadiliano katika mkuutano huu kwa kusema ulikuwa na maana kubwa kwa wawekezaji na wafanyabiashara kwani uliainisha changamoto zote na watusika ambaa ni serikali walitolea majibu au kufanyiwa kazi.

"Tunaimani mapendekezo yetu na Changamoto tulizowasilisha kwa viongozi wa serikali zitafanyiwa kazi kwa haraka ili kutoa nafasi kwa

mifanyabiashara na mwekezaji kunufaika na biashara yake na kuongeza hamasa ya kuanzisha viwanda zaidi," alisema Lema.